JUMUIYA YA TAWALA ZA MITAA TANZANIA

(ALAT)

Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC)

UBORESHAJI WA KIWANDA CHA USINDIKAJI WA ZAO LA MHOGO KUPITIA *BIG POWER GROUP* (KBPG)

KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO

Uzoefu Kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo

Kupitia *BIG POWER GROUP* (KBPG)

Kilichopo katika Mkoa wa Kigoma-Tanzania

Ripoti ya Mradi Imeandaliwa
na

Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT)
S.L.P. 2049
DODOMA

Imefadhiliwa na

Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC)

Kwa kushirikiana na

Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo
Agosti, 2018

YALIYOMO

NENO LA UTANGULIZI i
ORODHA YA VIFUPISHO ii
SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI 1
1.0. Usuli 1
1.1. Idadi ya Wakazi 2
1.2. Hali ya Hewa 2
1.3. Ufafanuzi Kuhusu Mradi 3
1.3.1. Wazo la Kuanzisha Mradi 3
1.3.2. Zao la Mhogo 5
1.4. Lengo la Mradi 7
1.4.1. Lengo Kuu 7
1.4.2. Malengo Mahususi 8
SURA YA PILI 9
SHUGHULI ZA MRADI, UTEKELEZAJI WA MIKAKATI, MIPANGO NA MAFANIKIO 9
2.0. Shughuli zilizotekelezwa 9
2.1. Utekelezaji wa Rasilimali 9
2.2. Matokeo na Mafanikio ya Mradi 10
SURA YA TATU 12
CHANGAMOTO, MAFUNZO NA MKAKATI 12
3.1. Mafunzo Muhimu Kutoka katika Mradi 12
3.2. Uendelevu wa Mradi 13
SURA YA NNE 14
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 14
4.0. Hitimisho 14
4.1. Mapendekezo 15

NENO LA UTANGULIZI

Andiko hili lenye jina Uimarishaji wa Mnyororo wa Thamani katika Zao la Mhogo katika Wilaya ya Kibondo, ni mfululizo wa maandiko kutoka ALAT yanayohusu miradi ya mfano chini ya udhamini wa Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC).

Andiko hili linaangazia juhudi za kikundi cha wakulima kiitwacho *Kibondo Big Power Group* (KBPG) ambacho madhumuni yake makubwa ni kuongeza mnyororo wa thamani ya zao la mhogo ili kukidhi mahitaji ya wateja wao. Andiko hili ni muhimu sana kwa wadau mbalimbali kama vile watunga sera, wataalamu wa mipango, watafiti, wafadhili na hata wakulima.

Mamlaka ya Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT) inaona kuwa hili ni jambo la muhimu linaloweza kusambazwa katika wilaya nyingine. Wasomaji wa andiko hili wanakaribishwa kutoa maoni yao na pia kulikosoa pale itakapobidi ili kuliimarisha na kuwa na tija kwa jamii.

Ninapenda kutumia nafasi hii kutambua umuhimu wa Ubalozi wa Denmark kwa msaada wao wa fedha kupitia mradi wa LIC ambao umewezesha kupatikana fedha za kuandaa na kuchapisha andiko hili. Shukrani maalumu ziende kwa mratibu wa mradi wa LIC, Bw. Flemming Winther Olsen na timu yake kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa mradi huu kwa kushirikiana na washikadau wa kitaifa kama vile Ofisi ya Waziri Mkuu, OR-TAMISEMI, TNBC, TPSF na TCCIA.

Pia, tunatoa shukrani kwa uongozi wa mkoa wa Kigoma, uongozi wa wilaya ya Kibondo na wakulima wa zao la mhogo chini ya mwamvuli wa KBPG kwa kutoa taarifa zilizosaidia kupatikana kwa andiko hili.

Mwisho, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa ALAT na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI hasa Bi. Husna A. Kandoro, Vicent Chomola na Anicetus Mramba kwa ukusanyaji wa taarifa zilizosaidia kupatiakana kwa andiko hili.



Abdallah S. Ngodu
Kaimu Katibu Mkuu– ALAT

ORODHA YA VIFUPISHO

ALAT	-	Association of Local Authorities of Tanzania
BTC	-	Belgian Technical Corporation (Development Agency)
DC	-	District Council
IITA	-	International Institute of Tropical Agriculture
KDC	-	Kibondo District Council
KBPG	-	Kibondo Big Power Group
LGA	-	Local Government Authorities
LIC	-	Local Investment Climate
PO- RALG	-	President's Office Regional Administration and Local Government
SIDO	-	Small Industries Development Organization
SIFF	-	Small Industrial Facilitation Fund
TBS	-	Tanzania Bureaua of Standards
TCCIA	-	Tanzania Chamber of Commerce, Industries and Agriculture
TNBC	-	Tanzania National Busness Council
TPSF	-	Tanzania Private Sector Foundation

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0. Usuli

Wilaya ya Kibondo ilianzishwa rasmi mnamo mwaka 1983 chini ya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa za Wilaya, kifungu Na. 7 cha mwaka 1982. Huko nyuma, Wilaya ya Kibondo ilitumika kama eneo maalumu la kuhifadhi wakimbizi kutoka nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemakrasia ya Watu wa Congo (DRC). Baadaye, mnamo mwaka 2013, Wilaya ya Kibondo iligawanywa na kupatikana Wilaya mpya ya Kakonko.

Wilaya ya Kibondo ipo Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Wilaya inapatikana baina ya latitudo 3.90 – 5.00 kwa upande wa Kusini na longitudo 30.20 – 31.500 kwa upande wa Mashariki. Kwa upande wa mwinuko, Wilaya hii ipo katika altitude 500m na 1,600m kutoka usawa wa bahari.

Kwa upande wa mipaka, Wilaya ya Kibondo inapakana na Wilaya ya Kakonko kwa upande wa Kaskazini, Wilaya ya Kaliua (Tabora) upande wa Mashariki, Wilaya ya Kasulu kwa upande wa Kusini na nchi ya Burundi kwa upande Magharibi. Kiutawala, Wilaya ya Kibondo ina Tarafa 3 ambazo ni Kibondo, Mabamba na Kifura. Aidha, Wilaya hii ina Kata 19, Vijiji 50, na Vitongoji na Mitaa 420.

Kabila kuu katika Wilaya ya Kibondo ni Waha, jina ambalo linatokana na asili ya mahali wanapotoka yaani Buha. Kwa asili, Kiha ni lugha ya Kibantu. Wengi hujishughulisha na kilimo kwa ajili biashara na chakula. Pia, hujihusisha na kufuga ng’ombe ambao ni alama muhimu katika sherehe za kitamaduni na mafungamano ya kijamii. Kihistoria, Waha wanasifika kwa kijihusisha na kazi za kufua vyuma. Makabila mengine yanayopatikana katika Wilaya ya Kibondo ni Wanyamwezi, Wasukuma, Wahaya, Wakurya, Wajita na Wanyakyusa.

1.1. Idadi ya Wakazi

Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Kibondo ilikuwa na wakazi 261,331 kati yao Wanaume 124,518 na Wanawake 136,813. Ongezeko la watu kwa mwaka ni asilimia 2.7. Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 37.3 ya idadi ya wakazi wana uwezo wa kufanya kazi. Wastani wa watu katika familia inakadiriwa kuwa ni watu watano. Aidha, wastani wa kuishi ni miaka 52. Kutokana na kuongezeka kwa watu kufika mwezi wa nane mwaka 2016 idadi ya watu iliongezeka na imekadiriwa kwasasa Wilaya ina wakazi 290,719 kati yao Wanaume ni 141,632 na Wanawake ni 149,719.

1.2. Hali ya Hewa

Wilaya ya Kibondo ina majira mafupi manne ya kiangazi. Mvua kubwa na za kati huanza mwezi wa kumi na wa tano. Mandhari ya Wilaya ni ya kitropiki wakati kiwango cha mvua ni kati ya milimita 800 hadi milimita 1,600 kwa mwaka. Wastani wa mvua ni milimita 1,000 na unyevu wa asilimia 10. Hali ya joto ni kati ya nyuzi joto 15°C– 22°C kwa mwaka mzima. Baridi kali hutokea kati ya mwezi wa Julai na Septemba kwa wastani wa nyuzi joto 15°C– 22°C.

Kwa upande wa Kilimo, Wilaya imegawika katika maeno matatu yafuatayo:

i) **Maeneo yenye mvua nyingi:** maeneo haya hufaa zaidi kwa mazao ya kawaida ya chakula kama vile kahawa, mahindi, mihogo, maharage, migomba na mazao ya mbogamboga.

ii) **Maeneo yenye mvua za wastani:** maeneo haya yapo katika uwanda wa kati baina ya mita 1,300– 1,600 kutoka usawa wa bahari na hupata mvua kwa wastani wa mm 1,000– 1,200mm. Uoto wa maeneo haya huwa ni mzuri kwa kilimo cha umwagiliaji. Wakazi wa maeneo haya hujishughulisha na kilimo cha karanga, mahindi, mhogo, maharage, migomba, tumbaku, mtama na uwele.

iii) **Maeneo yenye mvua kidogo:** eneo hili ni karibu mbili ya tatu ya eneo lote la Wilaya. Eneo lipo katika latitudo 1,000 hadi 1,200 kutoka usawa wa bahari. Kwa wastani mvua hunyesha kati ya mm 500– 750mm.

Kwa sehemu kubwa eneo hili ni mbuga yenye miti mingi ya miombo na hifadhi ya wanyama pori wengi kutokana na kuwepo kwa mbung'o. Shughuli kuu za kiuchumi katika eneo hili ni pamoja na kilimo, uwindaji, upasuaji mbao na urinaji asali. Mazao makuu yanayolimwa ni pamoja na mihogo, mtama, pamba na tumbaku na mengine yanayovumilia ukame. Kata ya Murungu ni mfano hai wa hali ya hewa inayopatikana katika eneo hili.

1.3. Ufafanuzi Kuhusu Mradi

KBPG ni kikundi cha Wakulima wa mihogo kilichopo katika Kijiji cha Kibondo Mjini, Kata ya Kibondo Mjini, umbali wa km 16 kutoka Mjini Kibondo. Eneo hili ni kati ya maeneo yenye mvua chache ambapo mazao yanayovumilia ukame hulimwa, mojawapo ya zao hilo ni mihogo. Kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2005 na mpaka sasa bado hakijasajiliwa rasmi.

Kwa ujumla, kikundi kilianza na wanachama 9 ambao ni wakulima wa mihogo na kwasasa kina wanachama 33, kati yao Wanaume ni 20 na Wanawake ni 13. Kikundi kinampokea mwanachama yeyote bila kujali jinsia, ulemavu, dini au sababu nyingine. Viongozi wa kikundi ni pamoja na Mwenyekiti, Matibu na Mweka Hazina. Viongozi hawa hukutana mara kwa mara kuzungumzia mambo mbalimbali yanayohusiana na Maendeleo ya Kilimo.

1.3.1. Wazo la Kuanzisha Mradi

Wazo la kuanzisha kikundi hiki lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, **Luteni Mstaafu Kanali John Mzurikwao** kufuatia hali iliyokuwepo kipindi hicho hasa suala la mwingiliano mkubwa wa wakimbizi wa kutoka DRC na Burundi. Kwa wakati huo kulikuwa na mwingiliano mkubwa wa wakimbizi halisi, wazururaji na wenyeji wa maeneo haya, hivyo ilikuwa ngumu kuwatenganganisha.

Kutokana na hali hii, Mkuu wa Wilaya alipendekeza kuundwa kwa vikundi vya uzalishaji mali. Inakadiriwa kuwa vijana kama 100,000 walijitokeza katika mradi huu. Vijana hawa walitakiwa kupendekeza shughuli za uzalishaji ambazo zingewaletea kipato.

Kwa kuzingatia kuwa shughuli kubwa inayofanyika katika Halmashauri ya Kibondo ni Kilimo, KGB iliamua kujikita katika kilimo. Mkuu wa Wilaya aliwapatia hekta 200. Aidha, Wilaya ilikamilisha taratibu zote za kisheria kuhusu umiliki wa Ardhi. Pia, Wilaya ilikipatia kikundi majembe ya mkono na mapanga tayari kwa kuanza shughuli za kilimo cha mihogo na mazao mengine ya biashara na chakula.



Kielezo Na. 1: Mchoro wa Shamba la KGB

Ili kuweza kutenganisha maeneo yanayolimwa aina mbalimbali ya mihogo, kikundi kiliotesha miti katika mipaka. Aidha, miti hii hutumika kama kinga ya moto. Mazao mengine yanayolimwa na kikundi ni Maparachichi hekari 33, Mpunga hekari 33, Miti hekari 120, Migomba hekari 4 na Korosho hekari 30.

Kielelezo Na. 2. ***Picha ya upande wa kushoto inaonesha aina mbalimbali ya mihogo ikiwa imetenganishwa na miti ya aina mbalimbali. Picha ya upande wa kulia inaonesha aina nyingine za mazao kama maparachichi na migomba.***

1.3.2. Zao la Mhogo

Mihogo ni zao la mizizi lenye kutupatia wanga ambalo hustawi ndani ya Ardhi. Mihogo huweza kukua na kufikia cm 15 hadi 100 na kuwa na uzito wa nusu kilo hadi kilo 2. Zao hili ni muhimu kwa chakula hasa kwenye maeneo yenye uhaba wa mvua. Aidha, zao hili lina uvumilivu wa magonjwa na hustawi katika maeneo yasiyo na rutuba. Mihogo huweza kukaa ardhini kwa miezi 18 baada ya kukomaa. Hivyo, ni zao muhimu kwa maeneo yenye ukame au misukosuko ya kisiasa.

Yapo matatizo mawili ambayo yanahusiana na uvunaji wa mihogo. Jambo la kwanza ni kuoza kwa mihogo mibichi baada tu ya kuvunwa. Jambo la pili ni matatizo ya kuwepo kwa "*cyanogenic compounds"* katika mihogo. Hali hii hujitokeza pale tu mihogo inapochimbwa na bila kutunzwa vizuri. Kwa mfano, mara nyingi mihogo hupata ukungu baada ya saa 48 baada ya kuchimbwa. Hali hii hupunguza thamani ya zao husika katika soko. Zao hili pia huweza kuharibika na kupata ukungu mzito kama litahifadhiwa katika mifuko ya plastiki/viroba.

Mihogo ina "*cyanogenic glucosides"*. Mara nyingi kama uvunaji na usindikaji wa mihogo usipofanyika kwa uangalifu huweza kusababisha madhara ya kiafya. Kwa kawaida "*cyanogenic glucosides"* huondoshwa kwa kumenya maganda na kuuloweka mhogo katika maji kwa muda fulani.

Ni wazi kuwa mihogo mibichi haina soko la uhakika na inaharibika kwa haraka. Kwa kawaida, soko la mihogo mibichi ni la ndani na bei yake ni ya chini sana. Kwa mfano, katika soko la ndani KBPG wamekuwa wakiuza mihogo iliyokaushwa kwa Shilingi 170 hadi 300 kwa kilo. Aidha, pamoja na uduni huu wa bei, mihogo iliyokaushwa au iliyosagwa na kuwa unga hudumu kwa muda mrefu, huweza kusafirishwa katika masoko ya mbali kwa malengo ya kutafuta bei nzuri zaidi.

Kwa hiyo, KBPG ni mdau muhimu katika kuongeza mnyororo wa thamani katika zao la mihogo. Hii ni kwa kuwa wao wanahusika sana katika usindikaji wa mihogo kutoka mihogo mibichi na kuwa unga wa mhogo au bidhaa nyingine. Mbali na kumiliki hekari 450 za mihogo, kikundi kimeanzisha viwanda vidogovidogo vya kusindika zao la mihogo. Pamoja na juhudi kubwa zilizofanywa na kikundi bado viwanda hivi havijakamilika (majengo na mashine).

Kutokamilika kwa viwanda hivi kumeleta changamoto kadhaa katika zoezi la usindikaji wa mihogo inayopatikana katika mradi. Hivyo basi, ili kuwezesha kukamilika kwa mnyororo wa thamani katika zao hili, KBPG iliamua kuomba msaada kutoka LIC ili kuwezesha kukamilisha ujenzi wa viwanda vitakavyowezesha usindikaji wa mazao yao.

Kielelezo Na. 3: Picha inayomuonesha Bw. Kennedy Salundari, Mweyekiti wa KBPG akiwa ameshika mfuko wenye unga wa mhogo katika moja ya kiwanda kilichofadhiliwa na LIC.

Kielelezo Na. 4: Picha za mashine mbili zinazotumika kusagia unga wa mihogo zinazofahamika kama *Cassava Grater*. Mashine moja ilinunuliwa na KBPG na ile ya pili imefadhiliwa na LIC.

1.4. Lengo la Mradi

Mradi huu umejumuisha lengo kuu na malengo mahususi

1.4.1. Lengo Kuu

Lengo kuu la mradi huu ni kuongeza thamani ya zao la mhogo kwa kuongeza soko na bei nzuri kupitia usindikaji/usagaji wa unga. Pia, mradi unalenga kuongeza muda wa kutumika kwa zao husika kwa minajili ya kuyafikia masoko yaliyopo mbali na eneo la mradi.

1.4.2. Malengo Mahususi

Mradi huu una malengo mahususi yafuatayo:

i. Kuboresha mbinu za kisasa za kilimo cha mihogo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa zao husika;

ii. Kubuni njia bora za kuongeza mnyororo wa thamani zitakazopunguza uwezekano wa mihogo kuharibika kabla haijasindikwa; na

iii. Kuanzisha masoko ya uhakika ya zao la mhogo litalowapatia wakulima bei nzuri.

SURA YA PILI

SHUGHULI ZA MRADI, UTEKELEZAJI WA MIKAKATI, MIPANGO NA MAFANIKIO

2.0. Shughuli zilizotekelezwa

Katika utekelezaji wa majukumu yake, kikundi cha KBPG kimefanya mambo yafuatayo:

1) Kununua na kufunga mashine za usindikaji mihogo na vifaa vyote vinavyohusika na utekelezaji wa mradi. Mashine zilizonunuliwa ni pamoja na *Chipper, Grater* na *Press and Sun Drier*;
2) Ununuzi wa matenki ya kuhifadhia maji;
3) Kukamilisha ujenzi wa vyumba vya kusindika mihogo;
4) Kuanza rasmi zoezi la usagaji wa unga wa mhogo na utengenezaji wa tambi zinazotokana na mhogo; na
5) Utafutaji wa masoko ya unga na mhogo pamoja na tambi.

2.1. Utekelezaji wa Rasilimali

Ufadhili uliotolewa na Mradi wa LIC ni Tsh. 25,850,000.00 (Milioni ishirini na tano laki nane na hamsini elfu). Mgawanyo wa fedha hizo zilitumika kama ifuatavyo:

a) Kununua mashine ya kusindika mihogo;
b) Kunua matenki mawili, moja likiwa na ujazo wa lita 10,000 na jingine lenye lita 1,000;
c) Mashine moja ya kusukuma maji;
d) Kununua marumaru/vigae 2,000;
e) *Cassava grater* moja;
f) *Cassava chipper* mbili;
g) Mashine ya kusagia mihogo moja;
h) Mashine ya kushonea mifuko/viroba;
i) Mashine ya moto ya kufungia mifuko/viroba;
j) Mashine ya kukaushia mhogo;
k) Mifuko 18 ya simenti ambayo gharama yake ni 342,000 (mifuko hii iligharamiwa na pesa za kikundi)

2.2. Matokeo na Mafanikio ya Mradi

Kikundi kimeonesha mafanikio makubwa katika kilimo cha mihogo ndani ya Wilaya ya Kibondo. Kikundi kilianza kilimo katika eneo lenye ukubwa wa hekari 26. Katika kipindi cha miaka mitatu kimeweza kuongeza kwa awamu ukubwa wa shamba na kufikia hekari 470.

Uzalishaji umeongezeka kutokea Tani moja kwa hekari na kufikia Tani tatu kwa hekari. Pia, mradi umekuwa ni sehemu muhimu ya shamba darasa ambalo hutumiwa na wadau mbalimbali wa kilimo kama vile Chuo cha Kilimo Ukiriguru na wadau wengine kutoka sehemu nyingine za nchi. Pia, mradi umekuwa ukitumika kama sehemu muhimu ya utayarishaji wa mbegu za mihogo ambayo hutumika ndani ya mradi na maeneo mengine ya nchi.

Mihogo inayolimwa katika mradi huu ni ile ambayo haishambuliwi sana na wadudu pamoja na maradhi mengine ya mazao. Aina ya mihogo inayolimwa katika mradi ni pamoja na mkombozi, meremeta, suma, kasara na Nigeria. Kwa kiasi kikubwa aina mbili ya mihogo, yaani mkombozi na meremeta ndiyo inayolimwa sana katika mradi kwa sababu hutoa mazao mazuri zaidi. Mbali na ujenzi wa kiwanda cha kusindika zao la mihogo kwa kushirikiana na LIC, KBPG imefanikiwa kufanya mambo yafuatayo:

i) Kuongeza uzalishaji wa zao la mhogo kutoka Tani 60 mwaka 2016/2017 na kufikia Tani 80 mwaka 2017/18.
ii) Kuongeza kipato cha wakulima. Kwa mfano, msimu wa mwaka 2013/14 kikundi kilipata Tsh 8,500,000/=. Msimu wa mwaka 2014/15 kikundi kilipata Tshs. 15,000,000/. Na msimu wa mwaka 2017/18 kikundi kilipata Tshs. 17,500,000/=.
iii) Kuinua kipato cha Kaya na hali za maisha ya wakulima kwa jumla. Kupitia kipato hiki wakulima wengi wameweza kuwalipia watoto wao ada za shule na kukidhi haja nyingine za kifamilia.
iv) Kuongeza ufahamu wa wakulima kupitia mafunzo na mijadala ya kitaalamu kwa kuwakutanisha na watu mbalimbali. Aidha, wakulima wameweza kushiriki katika shughuli mbalimbali za kitaifa kama vile maadhimisho ya wakulima (nane nane) yaliyofanyika mkoani Simiyu mwaka 2018.

v) Kuongezeka kwa imani kuhusu kikundi. Hali hii ni muhimu kwa maendeleo ya kikundi kwani kitawawezesha kupata misaada mbalimbali hasa ya kifedha kama ile iliyotolewa na LIC na KDC.

vi) Kuongezeka kwa ubora wa bidhaa zinazotengenezwa na KBPG. Hali hii imeongeza thamani na imewahakikishia wakulima kipato cha uhakika kutokana na kilimo cha mihogo. Bidhaa zinazotengenezwa ni pamoja na unga wa mhogo, tambi na chips.

Kielelezo Na. 5: Bidhaa kutoka KBPG inayofamika kama "Mpishi Mkuu". Bidhaa hii ipo tayari kwa kuuzwa na kuongeza kipato kwa wakulima.



Kielezo Na 6: Wanachama wa KBPG wakiwa wamebeba sehemu ya mazao ya mhogo kutoka katika mashamba yao.

SURA YA TATU

CHANGAMOTO, MAFUNZO NA MKAKATI

3.0. Changamoto

Katika uendeshaji wa shughuli za kila siku KBPG inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i) Kukosekana kwa umeme wa uhakika kwenye kiwanda cha usindikaji mihogo. Hali hii imesababisha uzalishaji kuchukuwa muda mrefu na gharama za uzalishaji kuongezeka;

ii) Kukosekana kwa huduma ya maji ya uhakika;

iii) Ukosefu wa vifaa vya kukaushia mihogo mibichi inayotoka shambani; na

iv) Ukosefu wa mota ya kufua umeme wa kuendesha mashine za kusagia unga wa mhogo.

3.1. Mafunzo Muhimu Kutoka katika Mradi

Wataalamu kutoka ALAT walipotembelea mradi wa KBPG na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo walijifunza mambo yafuatayo:

i) Mhogo unaweza kulimwa na mazao mengine mchanganyiko kama vile miti ya matunda na miti ya kawaida;

ii) Serikali kwa kutumia mfuko wa maendeleo wa Wilaya kwenye kilimo inaweza kuongeza mahusiano baina ya wakulima. Mahusiano haya yameifanya KBPG kuwa mfano mzuri kwa wakulima wengine;

iii) Suala la kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ni jambo la muhimu sana katika kukuza sekta ya kilimo; na

iv) Kilimo kina nafasi muhimu katika kuongeza fursa za ajira. Kupitia KBPG watu wengi wameajiriwa. Hali hii imepunguza sana wazururaji, wezi wa mifukoni na ombaomba waliokuwepo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

3.2. Uendelevu wa Mradi

Ili kuhakikisha kuwa jamii inafaidika kutokana na mradi na kuufanya mradi kuwa endelevu, kikundi kimejiwekea mikakati mbalimbali muhimu. Kama ilivyoelezwa huko nyuma, kikundi kina viongozi wa kuchaguliwa ambao ni Mwenyekiti, Katibu, Mhasibu na Muwezeshaji. Hadi sasa kikundi kina wanachama 33, kati yao wanachama 20 ni Wanaume na 13 ni Wanawake. Kwa pamoja viongozi hawa wanafanya shughuli zifuatazo:

i) Kuongoza vikao vinavyohusiana na shughuli za KBPG. Vikao hivi hulenga kujadili mafanikio, changamoto sanjari na njia za kutatua changamoto hizo;

ii) Kufanya mawasiliano na wadau, viongozi na Wilaya ya Kibondo, Mashirika ya Utafiti, kushiriki katika maonesho ya nanenane n.k kwa lengo la kuongeza uzoefu na kuongeza tija katika kikundi; na

iii) Kuendeleza kilimo cha mazao ya muda mfupi na mrefu ili kuongeza kipato cha kikundi na kupunguza gharama za uendeshaji wa mradi.

Wilaya ya Kibondo na hasa Idara ya Kilimo wameendelea kushirikiana kwa karibu na kikundi. Wadau wengine kama vile LITA, LIC, BTC, SIDO, watafiti kutoka Maruku, Ukiriguru na Naliendele wamendelea kuwa wadau muhimu wa mradi kwa kuwa wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu sana na wanakikundi.

SURA YA NNE

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

4.0. Hitimisho

KBPG ni kikundi ambacho hakijasajiliwa na kina Jumla ya wanachama 33. Malengo ya kikundi hiki ni pamoja na kujihusisha na kilimo cha mihogo, uuzaji wa mihogo mibichi pamoja na ile iliyosindikwa. Aidha, kikundi kina malengo ya kumalizia ujenzi wa kiwanda kidogo cha kusindika mazao ya mihogo pamoja na kukamilisha ununuzi wa vifaa muhimu vitakavyowezesha kiwanda kufanya kazi.

Katika utekelezaji wa shughuli zake, kikundi kimepata mafanikio mengi. Mafanikio hayo ni pamoja na kupata soko la uhakika kutoka mikoa ya karibu kama vile Shinyanga na Kagera. Pia, kikundi kinauza bidhaa zake katika nchi za Burundi, Congo, Uganda na Sudan ya Kusini.

Vilevile, kikundi kimepata fursa ya kushiriki katika maadhimisho ya Sherehe za Wakulima (nanenane) yaliyofanyika Kitaifa katika Mkoa wa Simiyu mnamo mwaka 2018. Aidha, uzalishaji wa mazao umeongezeka kutoka Tani 60 kwa msimu wa mwaka 2016/17 na kufikia Tani 80 kwa msimu wa mwaka 2017/18.

Kielelezo Na. 7: Banda la Halmashauri ya Wilaya Kibondo lililotumika kwa ajili kuonesha na kuuza bidhaa kutoka KBPG katika maonesho ya nanenane huko mkoani Simiyu mwaka 2018.

Pamoja na mafanikio mengi ya KBPG, kikundi kinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na uduni wa mazao yanayozalishwa ambayo hayaleti tija kwa mkulima. Ongezeko kubwa la gharama za uzalishaji linalotokana na ukosefu wa umeme na maji ya uhakika katika eneo la kiwanda.

4.1. Mapendekezo

Kulingana na hayo yaliyoelezwa hapo juu, ni wazi kuwa wakulima wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji juhudi za Serikali na wadau wengine katika kuzitatua. Hivyo basi, yafuatayo ni mapendekezo yatakayowezesha kuimarika kwa kilimo cha mihogo katika Wilaya ya Kibondo:

i) Kikundi hiki kama mdau mkubwa katika kilimo cha mihogo katika Wilaya ya Kibondo, kinapaswa kuimarisha suala la usindikaji wa mazao ya mihogo kwa manufaa ya kikundi;

ii) Wilaya ya Kibondo kinapaswa kuendelea kukisaidia kikundi hiki kwani ni mfano mzuri kwa vikundi vingine;

iii) Ushirikiano baina ya KBPG na LIC ni muhimu kuendelezwa kwa manufaa ya kikundi husika na jamii nzima ya wana-Kibondo; na

iv) Ni muhumu sana kwa Serikali Kuu kama mtengenezaji mkuu wa Sera kuandaa mazingira rafiki kwa vikundi vyenye malengo yanayoshabihiana na KBPG.

v) Vikundi hivi ni muhimu kwa kuongeza kipato katika ngazi ya Serikali za Mitaa kwani vinaongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya chakula na biashara.

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:
Katibu Mkuu Mtendaji wa ALAT
S. L. P. 2049
Simu: +255 784 514 245
Dodoma, Tanzania
Barua pepe: info@alat.or.tz
Tovuti: www.alat.or.tz